This script is intended to be used as a supplement to the Alt ELPA Test Administration Manual (TAM) and should be read aloud to students who would benefit from hearing the directions for administration read aloud in their home language. Test Administrators must read the complete TAM prior to using this document to ensure they are familiar with all the Alt ELPA test administration procedures. Note that some of the directions in this translation are only applicable to specific grade levels. Please consult the TAM and identify the directions you will need to read aloud prior to administering the test.

A recorded audio script of this translation will also be available. The tracks on the recorded script are listed in the first column of the table below.

## Practice Test—Student Login Instructions

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **1** | On your computer screen, locate the icon titled **SecureTest.** If you need help, alert me now and I will help you. | Kwenye skrini ya kompyuta yako, tafuta ikoni iitwayo **Secure Test**. Ukihitaji usaidizi, niarifu sasa niweze kukusaidia. |
| **2** | Double-click the **SecureTest** icon; the **Please Sign In** page will appear. Do not enter anything until you have been instructed to do so.<br><br>Can you see the **Please Sign In** page? If you cannot see the **Please Sign In** page, please let me know. | Bofyabofya ikoni ya **SecureTest**; ukurasa wa **Please Sign In (Tafadhali Ingia)** utatokea. Usiandike chochote hadi utakapoagizwa kufanya hivyo.<br><br>Unaweza Kuona ukurasa wa **Please Sign In (Tafadhali Ingia)**? Ikiwa huwezi kuona ukurasa wa **Pleae Sign In (Tafadhali Ingia)**, tafadhali niarifu. |
| **3** | Enter your first name, your SSID, and the Session ID and then click the **Sign In** button. If you need help let me know and I will help you. | Andika jina lako la kwanza, SSID yako, na Kitambulisho cha Kipindi kisha bofya kitufe cha **Sign In (Ingia).** Ukihitaji usaidizi niarifu niweze kukusaidia. |
| **4** | You should now see theIs **This You?** page. Make sure that the information on this page is correct. If the information is correct, click the **Yes** button . If the information is not correct click the **No** button. If you ne ed help let me know and I will help you. | Sasa unapaswa kuona ukurasa wa **Is This You (Huyu ni Wewe)?** Hakikisha kwamba taarifa zilizo katika ukurasa huu ni sahihi. Ikiwa taarifa hizi ni sahihi, bofya kitufe cha **Yes (Ndio)** . Ikiwa taarifa hizi si sahihi, bofya kitufe cha **No (La).** Ukihitaji usaidizi niarifu niweze kukusaidia. |
| **5** | You will now see the **Your Tests** page.Click on the link that says **Start ___________ Alt ELPA__________________Practice Test.** | Sasa utaona ukurasa wa **Your Tests (Mtihani Wako)**. Bofya kiungo kilichoandikwa **Start (Anza)** ___________ Alt ELPA__________________**Practice Test (Mtihani wa Majaribio).** |
| **6** | If you previously started a test but did not finish it, the **Resume** button will display next to the test name. Click the **Resume** button to resume the test. | Ikiwa ulikuwa umeanza mtihani awali ila hukuwa umeumaliza, kitufe cha **Resume** (Anza Tena) kitaonyeshwa kando ya jina la mtihani. Bofya kitufe cha **Resume (Anza Tena)** kuendelea na mtihani. |
| **7** | You should now see the **Choose Settings** screen. I will review your test settings. | Sasa unapaswa kuona skrini ya **Choose Settings (Chagua Mipangilio)**. Nitapitia mipangilio ya mtihani wako. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **8** | You should now see the **Audio/Video Checks** screen. | Sasa unapaswa kuona skrini ya **Audio/Video Checks (Ukaguzi wa Sauti/Video)**. |
| **9** | Under **Audio Playback Check**, click on the **Sound** button to hear the sound. If you hear the sound, click the **I heard the sound** button. A checkmark will appear in the top right-hand corner of the window.<br>If you do not hear the sound, let me know and I will help you. | Chini ya **Audio Playback Check (Ukaguzi wa Sauti)**, bofya kitufe cha **Sound** (Sauti) ili kusikia sauti. Ukiisikia sauti, bofya kitufe cha **I heard the sound (Nimeisikia Sauti)**. Alama ya mkwaju itaonekana katika kona ya juu kulia ya skrini. Ikiwa hutaisikia sauti, niarifu nikusaidie. |
| **10** | Now click the **Continue** button at the bottom of the screen. | Sasa bofya kitufe cha **Continue (Endelea)** upande wa chini wa skrini. |
| **11** | You should now see the **Instructions and Help** screen. Click on the **View Help Guide** button. Does everyone see the Help Guide? If you do not see the **Help Guide,** let me know an d I will help you. | Sasa unapaswa kuona skrini ya **Instructions and Help (Maagizo na Usaidizi).** Bofya kitufe cha **View Help Guide (Tazama Mwongozo)**. Je kila mtu anaona **Help Guide (Mwongozo)**? Ikiwa huoni **Help Guide (Mwongozo)**, niarifu nikusaidie. |
| **12** | The **Help Guide** has important information about moving through the test, pausing the test, and the tools available for this test. | **Help Guide (Mwongozo)** una taarifa muhimu kuhusu kuutalii mtihani, kusitisha mtihani na zana zilizopo kwa ajili ya mtihani. |
| **13** | Look at the **Tool Button Sheet** that I just passed out. You will follow along with me as I explain the buttons and tools you will see and use during the test. You will only listen to me while looking at the sheet, you will not be using your computer at this time. If you have a question while I am reviewing this tool sheet with you, let me know. | Tazama **Tool Button Sheet (Ukurasa wa Vitufe vya Zana)** ambayo nimetuma sasa hivi. Utanifuata ninapoeleza kuhusu vitufe na zana utakazoona na kutumia wakati wa mtihani. Utanisikiliza tu huku ukiangalia skrini, hutatumia kompyuta yako wakati huu. Ukiwa na swali wakati ninaendelea kupitia ukurasa wa zana pamoja na wewe, niarifu. |
| **14** | Look at row 1. You may click on the **Question Mark** button in the top right-hand corner of your screento see the *Online Test Directions* at any time. | Tazama safu ya 1. Unaweza kubofya kitufe cha Question Mark **(Alama ya Kiulizi)** kwenye kona ya juu kulia ya skrini ili kuona Maelekezo ya Mtihani wa Mtandaoni wakati wowote. |
| **15** | Look at row 2. Click on the **X** button in the upper right-handside of the **Help Guide** pop-up window to close the **Help Guide**. | Tazama safu ya 2. Bofya kitufe cha **X** kwenye sehemu ya juu upande wa kulia wa skrini inayojitokeza ya H**elp Guide (Mwongozo)** ili kufunga **Help Guide (Mwongozo)**. |
| **16** | Look at row 3. Click on the **Zoom In** button to make the text and images bigger. Click on the **Zoom Out** button to make the text and images smaller. There are four zoom levels. | Tazama safu ya 3. Bofya kitufe cha **Zoom In (Zumishia Ndani)** ili kukuza maandishi na picha. Bofya kitufe cha **Zoom Out (Zumishia Nje)** ili kupunguza maandishi na picha. Kuna viwango vinne vya zumu. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **17** | Look at row 4. Click the **Question Drop-Down List** to move to a different question on the test. | Tazama safu ya 4. Bofya **Question Drop-Down List (Kiashiria cha Orodha ya Maswali)** ili kusonga kwenda swali jingine la mtihani. |
| **18** | Look at row 5. Click the **Save** button to save work when answering a question. Your answers are saved automatically when you move to another question. You do not have to use the Save button for your answers to be saved. | Tazama safu ya 5. Bofya kitufe cha **Save (Hifadhi)** ili kuhifadhi kazi unapojibu swali. Majibu yako yanahifadhiwa kiotomatiki unaposonga kwenda katika swali jingine. Si lazima utumie kitufe cha **Save (Hifadhi)** kuhifadhi jibu lako. |
| **19** | Look at row 6. You will click the **Pause** button to exit the test before finishing.If you **Pause** the test, you will be logged out. Always check with your test administrator(s) before clicking the **Pause** button. | Tazama safu ya 6. Utabofya kitufe cha **Pause (Tua)** kuondoka kutoka kwenye mtihani kabla ya kuukamilisha. Kama utabofya **Pause (Tua)** wakati wa mtihani, utaondolewa nje. Mara zote shauriana na msimamizi wako wa mtihani kabla ya kubofya kitufe cha **Pause (Tua)**. |
| **20** | Look at row 7. After you answer a question, you will click the **Next** button to go to the next question or screen. | Tazama safu ya 7. Baada ya kujibu swali, utabofya kitufe cha **Next (Ifuatayo)** kwenda katika swali au skrini inayofuata. |
| **21** | Look at row 8. Click the **Back** button to go back to the previous question or screen. | Tazama safu ya 8. Bonyeza kitufe cha **Back (Nyuma)** kwenda katika swali au skrini iliyotangulia. |
| **22** | Look at row 9. When you have finished all the test questions, you will click the **End Test** button to end your test. The **End Test** button will only show on the screen when you reach the last question in the test. Always check with your test administrator(s)before clicking the **End Test** button. | Tazama safu ya 9. Utakapomaliza kujibu maswali yote, utabofya kitufe cha **End Test (Tamatisha Mtihani)** ili kutamatisha mtihani wako. Kitufe cha **End Test (Tamatisha Mtihani)** kitaonekana tu kwenye skrini utakapofikia swali la mwisho kwenye mtihani. Mara zote shauriana na msimamizi wako wa mtihani kabla ya kubofya kitufe cha **End Test (Tamatisha Mtihani)**. |
| **23** | Look at row 10. Click the **Expansion Tool** button during the reading test to make the left or right side of the screen smaller or larger. | Tazama safu ya 10. Bofya kitufe cha **Expansion Tool (Kikuza Maandishi)** wakati wa mtihani wa kusoma ili kupanua au kupunguza upande wa kulia au kushoto wa skrini. |
| **24** | Look at row 11. Click the **Unanswered Question Flag** button to return to any unanswered questions in the test. | Tazama safu ya 11. Bofya kitufe cha **Unanswered Question Flag** (Kibendera cha Maswali Hayajajibiwa) kurejelea swali lolote ambalo halikujibiwa kwenya mtihani. |
| **25** | Look at row 12. Click the **Replay** button to replay any directions or text that was previously played. | Tazama safu ya 12. Bofya kitufe cha **Replay (Rudia Tena)** ili kuonyesha upya maelekezo au maandishi yaliyoonyeshwa awali. |
| **26** | Look at row 13. Click the **Context Menu** button to access tools like the **Notepad,** | Tazama safu ya 13. Bofya kitufe cha **Context Menu (Menyu ya Muktadha)** |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| | **Mark/Unmark for Review**, **Highlighter**, and **Strikethrough** option. | kupata zana kama vile **Notepad (Kitini), Mark/Unmark for Review** (Tenga/Ondoa Kupitia), **Highlighter (Kiangaza)**, na **Strikethrough (Kipiga Mstari)**. |
| **27** | Look at row 14. Click the **Notepad** button to type notes to yourself about a passage or question, then click **Save and Close**. A picture of a **Pencil with a check mark** will show next to the questions with student notes. | Tazama safu ya 14. Bofya kitufe cha **Notepad (Kitini)** kujiandikia vidokezo kuhusu kifungu au swali, kisha bofya **Save and Close (Hifadhi na Kufunga).** Picha ya **Pencil (Penseli)** iliyo na mkwaju itatokea kando ya maswali yaliyo na vidokezo vya mwanafunzi. |
| **28** | Look at row 15. Click the **Mark for Review** button for questions that you want to look at again later. The box around the question number changes to shows a **Corner Flap** and a picture with a **Marked for Review Flag.** | Tazama safu ya 15. Bofya kitufe cha **Mark for Review (Tenga Kupitia)** kwenye maswali ambayo ungependa kupitia upya baadaye. Kisanduku cha nambari ya swali hubadilika kuonyesha **Corner Flap (Bapa la Kona)** na picha yenye **Marked for Review Flag (Kibendera chaTenga Kupitia).** |
| **29** | Look at row 16. Click the **Highlight Selection** button to highlight words. Click the **Remove Highlight** button to remove some highlighting. Click the **Reset Highlighting** to remove all highlighting. | Tazama safu ya 16. Bofya kitufe cha **Highlight Selection** kuangazia maneno. Bofya kitufe cha **Remove Highlight** kuondoa rangi katika baadhi ya maneno yaliyoangaziwa. Bofya kitufe cha **Reset Highlighting** kuondoa rangi katika maneno yote yaliyoangaziwa. |
| **30** | Look at row 17. Click the **Strikethrough** button on multiple choice questions to get rid of answer choices not needed. | Tazama safu ya 17. Bofya kitufe cha **Strikethrough (Kipiga Mstari)** katika maswali ya kuchagua majibu ili kuondo majibu yasiyohitajika. |
| **31** | Look at row 18. You may use the **Hand Pointer** button to select some information on the toolbar. | Tazama safu ya 18. Unaweza kutumia kitufe cha **Hand Pointer** (**Kiashiria ch**a **Mkono)** kuchagua baadhi ya taarifa katika mwambaa zana. |
| **32** | Do you have any questions about the Tool Button Sheet? | Je, una maswali yoyote kuhusu Tool |
| **33** | Before we begin the test remember to read each question carefully and think about what the question is asking you to do. If the test question has pictures, look carefully at pictures because they may help you understand the question. | Kabla tuanze mtihani kumbuka kusoma kila swali kwa makini na kufikiri kuhusu mahitaji ya swali. Ikiwa swali lina picha, tazama picha hizo kwa makini kwa sababu zitakusaidia kulielewa swali. |
| **34** | For responses that have to be written, type your answers in the space provided on the screen. For multiple-choice questions, click on the answer you choose. To change an answer, just click on a different answer. Always try your best and choose the answer that makes the most sense to you. | Katika majibu ambayo yatahitajika kuandikwa, yaandike majibu yako katika nafasi iliyotolewa kwenye skrini. Kwenye maswali yenye majibu ya kuteua, bofya jibu ulilochagua. Ukitaka kubadilisha jibu, bofya tu jibu unalolitaka. Mara zote jitahidi |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| | Do you have any questions? | kuchagua jibu ambalo lina mantiki zaidi kwako. Una maswali yoyote? |
| **35** | When you are ready to begin the practice test, click the **Begin Test Now** button. | Ukiwa tayari kuanza mtihani wa majaribio, bofya kitufe cha **Begin Test Now (Anza Mtihani Sasa)**. |
| **36** | You should now see the **Attention** box that asks you to select the **End Test** button to review your answers. Click **OK** and then the **End Test** button with the red square at the top of your screen. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Attention (Tahadhari)** kinachokuomba uchague kitufe cha **End Test (Tamatisha Mtihani)** ili kuyapitia majibu yako. Bofya kitufe cha **OK** kisha **End Test (Tamatisha Mtihani)** kilicho na mraba mwekundu juu ya skrini yako. |
| **37** | If you are using full screen, select  in the upper-left corner to exit full-screen mode and access the global menu. A message appears, asking for a password. Enter your first name as password and select **OK.** The global menu appears on the top of the screen. | Kama unatumia skrini nzima, chagua  katika kona ya juu kushoto kuondoka kutoka skrini nzima na kuifikia menyu ya dunia. Ujumbe utakuokuomba nenosiri utajitokeza. Andika jina lako la kwanza kama nenosiri kisha bofya **OK**. Menyu ya dunia itatokea sehemu ya juu ya skrini. |
| **38** | You should now see another **Attention** box saying you have reached the end of the test. Click the **Yes** button. | Unapaswa sasa kuona kisanduku kingine cha **Attention (Tahadhari)** kinachosema umefika mwisho wa mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)**. |
| **39** | If you have marked any items for review, please go back and check these items now. You will not be able to go back to these questions later. | Kama ulitenga maswali mengine kuyapitia baadaye, tafadhali yapitie sasa. Hutaweza kuyarudia maswali haya baadaye. |
| **40** | If you are sure that you are done with all the questions in this test, please select the **Submit Test** button. | Kama una uhakika kwamba umekamilisha maswali yote katika mtihani huu, tafadhali bofya kitufe cha **Submit Test (Wasilisha Mtihani)**. |
| **41** | You should now see a **Warning** box asking if you are sure you want to submit the test. Click the **Yes** button if you are done. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Warning (Onyo)** kikiuliza kama una uhakika unataka kuwasilisha mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)** ikiwa umemaliza. |
| **42** | You will now see the **Your Results** page. You may click the **Log Out** button now. This screen does not give us any test results. It just confirms that your test was completed and submitted, and is now moving on to be scored. | Sasa utaona ukurasa wa **Your Results (Matokeo Yako)**. Unaweza kubofya kitufe cha **Log Out (Ondoka)** sasa. Skrini hii haitupatii matokeo yoyote ya mtihani. Inathibitisha tu kwamba mtihani wako ulikamilishwa na kutumwa na sasa unaelekezwa hatua ya kutuzwa alama. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

## SUMMATIVE ASSESSMENT—STUDENT LOGIN INSTRUCTIONS

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| 1 | On your computer screen, locate the icon titled **SecureTest.** Double-click this icon and the program will launch. If you need help, let me know and I will help you. | Kwenye skrini ya kompyuta yako, tafuta ikoni iitwayo **Secure Test.** Bofyabofya ikoni hii na programu itafunguka. Ukihitaji usaidizi, niarifu niweze kukusaidia. |
| 2 | Once the program has opened, you will see the **Student Sign In** page. Do not enter anything until you have been instructed to do so. Can you see the **Student Sign In** page? If you need help, please let me know and I will help you. | Pindi tu programu itakapofunguka, utaona ukurasa wa **Student Sign In (**Mwanafunzi Kuingia). Usiandike chochote hadi utakapoagizwa kufanya hivyo. Unaona ukurasa wa **Student Sign In (Mwanafunzi Kuingia**)? Ukihitaji usaidizi, tafadhali niarifu niweze kukusaidia. |
| 3 | Type your first name into the field titled **First Name.** | Andika jina lako la kwanza katika eneo la **First Name (Jina la Kwanza).** |
| 4 | Now click on the SSID field. Type in your **Student ID** number. | Sasa bofya eneo la SSID. Ingiza nambari yako ya **Student ID (Kitambulisho cha Mwanafunzi)**. |
| 5 | Now click on the **Session ID** field. Type in the Session ID I have written on the board.If you need help, let me know a  nd I will help you. | Sasa bofya eneo la **Session ID (Kitambulisho cha Kipindi)**. Ingiza Kitambulisho cha Kipindi nilichoandika ubaoni. Ukihitaji usaidizi, niarifu niweze kukusaidia. |
| 6 | Click the **Sign In** button at the bottom of the pageto start the test. | Bofya kitufe cha **Sign In (Ingia)**  katika sehemu ya chini ya ukurasa ili kuanza mtihani. |
| 7 | Now you should see **Is This You?** screen. Do you see your name on the screen? If you do not see your own name, or if your name is not spelled correctly, let me know. | Sasa Unapaswa kuona skrini ya **Is This You (Huyu ni Wewe)?** Unaona jina lako kwenye skrini? Kama huoni jina lako, au kama jina lako halijaandikwa vizuri, niarifu. |
| 8 | Now make sure that the rest of the information on your screen is correct.<br>• your Grade<br>• your SSID<br>• your School<br>If any of the information is not correct, please let me know. If all of the information is correct, you can click the **Yes** button at the bottom of the screen. Do not go past the next screen until I tell you to. | Sasa hakikisha kwamba taarifa nyingne zote kwenye skrini ziko sahihi.<br>• Gredi yako<br>• SSID yako<br>• Shule yako<br>Kama taarifa yoyote si sahihi, tafadhali niarifu. Kama taarifa zote ziko sahihi, unaweza kubofya kitufe cha **Yes (Ndio)** sehemu ya chini ya skrini. Usisonge kwenda skrini inayofuata hadi nitakapokwambia. |
| 9 | Now we are going to begin the test. Click on the link that says **Start Grades__________Alt** | Sasa tunaanza mtihani. Bofya kiungo kilichoandikwa **Start Grades (Anza Gredi)__________Alt** |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| | **ELPA__________________ Test.** If you need help, let me know and I will help you. | **ELPA__________________ Test (Mtihani).** Ukihitaji usaidizi, niarifu niweze kukusaidia. |
| **10** | If you previously started a test but did not finish it, the link will say **Resume Grades_____ Alt ELPA Test.** | Ikiwa ulikuwa umeanza mtihani awali ila hukuwa umeumaliza, kiungo kitaandikwa **Resume Grades (Anza Tena Gredi)**_____ Alt ELPA Test (Mtihani wa Alt ELPA). |
| **11** | You should now see the **Audio/Video Checks** screen. | Sasa unapaswa kuona skrini ya **Audio/Video Checks (Ukaguzi wa Sauti/Video)**. |
| **12** | Under **Audio Playback Check**, click on the **Sound** button to hear the sound. If you hear the sound, click **I heard the sound**. A checkmark will appear in the top right-hand corner of the window.<br><br>If you do not hear the sound, let me know. | Chini ya **Audio Playback Check (Ukaguzi wa Sauti)**, bofya kitufe cha **Sound (Sauti)** ili kusikia sauti. Ukiisikia sauti, bofya kitufe cha **I heard the sound (Nimeisikia Sauti)**. Alama ya mkwaju itaonekana katika kona ya juu kulia ya skrini.<br><br>Ikiwa hutaisikia sauti, niarifu. |
| **13** | Click the **Continue** button to move to the next screen. | Bofya kitufe cha **Continue** (**Endelea)** ili kusonga kwenda skrini inayofuata. |
| **14** | You should now see the **Instructions and Help** screen. Does everyone see the instructions? If you do not see the instructions, please let me know. | Sasa unapaswa kuona skrini ya **Instructions and Help (Maagizo na Usaidizi).** Je kila mtu anaona maagizo? Ikiwa huoni maagizo, tafadhali niarifu. |
| **15** | This screen contains the same information about the tool buttons as you saw in the practice test. You can access these instructions at any time during the test by clicking on the **Question Mark** button in the top right-hand corner of your screen. | Skrini hii ina taarifa kuhusu vitufe vya zana sawa na ulivyoona katika mtihani wa majaribio. Unaweza kufikia maagizo haya wakati wowote wa mtihani kwa kubofya kitufe cha **Question Mark (Alama ya Kiulizi)** katika kona ya juu kulia ya skrini yako. |
| **16** | Do you have any questions about the **Instructions and Help** screen? | Je una maswali yoyote kuhusu skrini ya **Instructions and Help (Maagizo na Usaidizi).** |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

## SUMMATIVE ASSESSMENT–DIRECTIONS FOR ADMINISTRATION: LISTENING

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **1** | This is a Listening test. It will give you a chance to show how well you can listen to and understand English. You will hear things like conversations and presentations. Listen carefully. If you need to hear the conversation or presentation again, click on the **Replay** button.<br>It will also be read to you. You can hear a question again by clicking on the **Replay** button beside the question. If you want to hear a response read to you, click on the **Replay** button beside that response. Some questions you will answer by dragging and dropping an object or a word. You can change your answer by dragging the object to a different place or by dragging a different object. Other questions you will answer by clicking on the response. You can change your answer by clicking on a different response. Do you have any questions? | Huu ni mtihani wa Kusikiliza. Utakupa fursa ya kuthibitisha ubora wa usikilizaji na uelewa wako wa Kiingereza. Utasikia masuala kama vile mazungumzo na mawasilisho. Sikiliza kwa makini. Ukitaka kusikia tena mazungumzo au mawasilisho, bofya kitufe cha **Replay (Rudia Tena)**.<br>Pia utasomewa haya yote. Unaweza kusikiza swali tena kwa kubofya kitufe cha **Replay (Rudia Tena)** kilicho kando ya swali. Ukitaka kusomewa jibu, bofya kitufe cha **Replay (Rudia Tena)** kilicho kando ya jibu. Utayajibu maswali mengine kwa kukokota na kudondosha vitu au maneno. Unaweza kubadilisha jibu kwa kukokota kitu hadi sehemu tofauti au kwa kukokota kitu tofauti. Maswali mengine utayajibu kwa kubofya juu ya majibu. Unaweza kubadilisha jibu kwa kubofya kwenye jibu tofauti. Una maswali yoyote? |
| **2** | Try to answer all test questions. Keep working until you reach the end of the test. Once you finish, you may check your work in this test only. Remember, you can see the directions whenever you need them during the test by clicking the **Question Mark** button in the top right-hand corner of your screen. | Jaribu kujibu maswali yote ya mtihani. Endelea kujibu maswali hadi ufike mwisho wa mtihani. Pindi unapomaliza kujibu maswali, unaweza kukagua kazi yako katika mtihani huu pekee. Kumbuka, unaweza kuona maelekezo unapoyahitaji wakati wa mtihani kwa kubofya kitufe cha **Question Mark (Alama ya Kiulizi)** katika kona ya juu kulia ya skrini yako. |
| **3** | When you reach the **Attention** box saying that you have answered all the questions on this test, do not go on, please let me know,and I will help you. When you are ready to begin this test, click the **Begin Test Now** button. | Ukifikia kisanduku cha **Attention (Tahadhari)** kinachokuarifu kwamba umejibu maswali yote katika mtihani huu, usiendelee, tafadhali, niarifu nikusaidie. Ukiwa tayari kuanza mtihani huu, bofya kitufe cha **Begin Test Now (Anza Mtihani Sasa)**. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **4** | You should now see the **Attention** box that asks you to select the **End Test** button to review your answers. Click **OK** and then the **End Test** button with the red square at the top of your screen. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Attention (Tahadhari)** kinachokuomba uchague kitufe cha **End Test (Tamatisha Mtihani)** ili kuyapitia majibu yako. kitufe cha **OK** kisha **End Test (Tamatisha Mtihani)** kilicho na mraba mwekundu juu ya skrini yako. |
| **5** | If you are using full screen, select  in the upper-left corner to exit full-screen mode and access the global menu. A message appears, asking for a password. Enter your first name as password and select **OK.** The global menu appears on the top of the screen. | Kama unatumia skrini nzima, chagua  katika kona ya juu kushoto kuondoka kutoka skrini nzima na kuifikia menyu ya dunia. Ujumbe utakuokuomba nenosiri utajitokeza. Andika jina lako la kwanza kama nenosiri kisha bofya **OK**. Menyu ya dunia itatokea sehemu ya juu ya skrini. |
| **6** | You should now see another **Attention** box saying you have reached the end of the test. Click the **Yes** button. | Unapaswa sasa kuona kisanduku kingine cha **Attention (Tahadhari)** kinachosema umefika mwisho wa mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)**. |
| **7** | If you have marked any items for review, please go back and check these items now. You will not be able to go back to these questions later. | Kama uliweka kando maswali mengine ya kuyapitia baadaye, tafadhali yapitie sasa. Hutaweza kuyarudia maswali haya wakati mwingine. |
| **8** | If you are sure that you are done with all the questions in this test, please select the **Submit Test** button. | Kama una uhakika kwamba umekamilisha maswali yote katika mtihani huu, tafadhali bofya kitufe cha **Submit Test (Wasilisha Mtihani)**. |
| **9** | You should now see a **Warning** box asking if you are sure you want to submit the test. Click the **Yes** button if you are done. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Warning (Onyo)** kikiuliza kama una uhakika unataka kuwasilisha mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)** ikiwa umemaliza. |
| **10** | You will now see the **Your Results** page. You may click the **Log Out** button now. This screen does not give us any test results. It just confirms that your test was completed and submitted, and is now moving on to be scored. | Sasa utaona ukurasa wa **Your Results (Matokeo Yako)**. Unaweza kubofya kitufe cha **Log Out (Ondoka)** sasa. Skrini hii haitupatii matokeo yoyote ya mtihani. Inathibitisha tu kwamba mtihani wako ulikamilishwa na kutumwa na sasa unaelekezwa hatua ya kutuzwa alama. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

## Summative Assessment–Directions For Administration: Reading

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **1** | This is a Reading test; it will give you a chance to show how well you can read and understand English. | Huu ni mtihani wa Kusoma; utakupa fursa ya kuthibitisha ubora wa usomaji na uelewa wako wa Kiingereza. |
| **2** | Some questions are about a story. You will read along as you listen to the story. Then you will answer the questions.<br><br>You will answer some questions by clicking on a picture. You will answer other questions by clicking on some words. It is easy to change an answer if you change your mind. Just click on a different picture or different words.<br><br>You will also answer questions by moving a word or picture. You can change your answer by moving the word to a different place or moving a different picture.<br><br>If you have a question, or do not understand what to do, please let me know. | Maswali mengine yanahusu kusikiliza hadithi. Utasoma sambamba na kusikiliza hadithi. Kisha utajibu maswali kadhaa.<br><br>Utajibu maswali mengine kwa kubofya kwenye picha. Utajibu maswali mengine kwa kubofya kwenye maneno. Ni rahisi kubadilisha jibu lako kama utabadilisha mawazo yako. Bofya tu kwenye picha au maneno tofauti.<br><br>Pia utajibu maswali kwa kusogeza neno au picha. Unaweza kubadilisha jibu lako kwa kusogeza neno kwenda sehemu nyingine au kusogeza picha tofauti.<br><br>Kama una swali, au hufahamu cha kufanya, tafadhali niarifu. |
| **3** | Some questions are about a passage. Read the passage first before you try to answer the questions.<br><br>You will answer some questions by dragging and dropping words. You can change your answer by dragging the words to a different place, or by dragging different words. | Maswali mengine yanahusu usomaji wa kifungu. Soma kwanza kifungu kabla ya kujaribu kujibu maswali.<br><br>Utajibu maswali mengine kwa kukokota na kudondosha maneno. Unaweza kubadilisha jibu lako kwa kukokota maneno kwenda sehemu nyingine, au kwa kukokota maneno tofauti. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| | You will answer other questions by clicking on words, pictures, or sentences. You can change your answer by clicking on different words, pictures, or sentences.<br><br>If you have a question, or do not understand what to do, please let me know. | Utajibu maswali mengine kwa kubofya kwenye maneno, picha, au sentensi. Unaweza kubadilisha jibu lako kwa kubofya kwenye maneno, picha, au sentensi tofauti.<br>Kama una swali, au hufahamu cha kufanya, tafadhali niarifu. |
| **4** | Try to answer all test questions. Keep working until you reach the end of the test. Once you finish, you may check your work in this test only. Remember, you can see the directions whenever you need them during the test by clicking the **Question Mark** button in the top right-hand corner of your screen. | Jaribu kujibu maswali yote ya mtihani. Endelea kujibu maswali hadi ufike mwisho wa mtihani. Pindi unapomaliza kujibu maswali, unaweza kukagua kazi yako katika mtihani huu pekee. Kumbuka, unaweza kuona maelekezo wakati wowote mtihani unapoendelea kwa kubofya kitufe cha **(Alama ya Kiulizi)** katika kona ya juu kulia ya skrini yako. |
| **5** | When you reach the **Attention** box saying that you have answered all the questions on this test, do not go on, please let me know and I will help you. When you are ready to begin this test, click the **Begin Test Now** button. | Ukifikia kisanduku cha **Attention (Tahadhari)** kinachokuarifu kwamba umejibu maswali yote katika mtihani huu, usiendelee, tafadhali, niarifu nikusaidie. Ukiwa tayari kuanza mtihani huu, bofya kitufe cha **Begin Test Now (Anza Mtihani Sasa)**. |
| **6** | You should now see the Attention box that asks you to select the **End Test** button to review your answers. Click **OK** and then the **End Test** button with the red square at the top of your screen. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Attention (Tahadhari)** kinachokuomba uchague kitufe cha **End Test (Tamatisha Mtihani)** ili kuyapitia majibu yako. Bofya kitufe cha **OK** kisha **End Test (Tamatisha Mtihani)** kilicho na mraba mwekundu juu ya skrini yako. |
| **7** | If you are using full screen, select  in the upper-left corner to exit full-screen mode and access the global menu. A message appears, asking for a password. Enter your first name as password and select **OK.** The global menu appears on the top of the screen. | Kama unatumia skrini nzima, chagua  katika kona ya juu kushoto kuondoka kutoka skrini nzima na kuifikia menyu ya dunia. Ujumbe utakuokuomba nenosiri utajitokeza. Andika jina lako la kwanza kama nenosiri kisha bofya **OK**. Menyu ya dunia itatokea sehemu ya juu ya skrini. |
| **8** | You should now see another **Attention** box saying you have reached the end of the test. Click the **Yes** button. | Unapaswa sasa kuona kisanduku kingine cha **Attention (Tahadhari)** kinachosema umefika mwisho wa mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)**. |
| **9** | If you have marked any items for review, please go back and check these items now. You will not be able to go back to these questions later. | Kama uliweka kando maswali mengine ya kupitia baadaye, tafadhali yapitie sasa. Hutaweza kuyarudia maswali haya wakati mwingine. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **10** | If you are sure that you are done with all the questions in this test, please select the **Submit Test** button. | Kama una uhakika kwamba umekamilisha maswali yote katika mtihani huu, tafadhali bofya kitufe cha **Submit Test (Wasilisha Mtihani)**. |
| **11** | You should now see a **Warning** box asking if you are sure you want to submit the test. Click the **Yes** button if you are done. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Warning (Onyo)** kikiuliza kama una uhakika unataka kuwasilisha mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)** ikiwa umemaliza. |
| **12** | You will now see the **Your Results** page. You may click the **Log Out** button now. This screen does not give us any test results. It just confirms that your test was completed and submitted, and is now moving on to be scored. | Sasa utaona ukurasa wa **Your Results (Matokeo Yako)**. Unaweza kubofya kitufe cha **Log Out (Ondoka)** sasa. Skrini hii haitupatii matokeo yoyote ya mtihani. Inathibitisha tu kwamba mtihani wako ulikamilishwa na kutumwa na sasa unaelekezwa hatua ya kutuzwa alama. |

## Summative Assessment–Directions For Administration: Writing

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **1** | This is a Writing test. It will give you a chance to show how well you can write in English. | Huu ni mtihani wa Kuandika. Utakupa fursa ya kuthibitisha uwezo wako wa kuandika kwa Kiingereza. |
| **2** | Some questions will ask you to make words or sentences by dragging and dropping letters or words. | Maswali mengina yatakutaka uunde maneno au sentensi kwa kukokota na kudondosha herufi au maneno. |
| **3** | Other questions will ask you to type your answer. There will be a box for you to type in. | Maswali mengine yatakutaka uandike majibu yako. |
| **4** | Some questions will ask you to choose the right word to finish a sentence by clicking on the word. Other questions will ask you to type | Maswali mengine yatakutaka uchague neno sahihi kukamilisha sentensi kwa kulibofya neno hilo. Maswali mengine |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| | your answer. There will be a box for you to type in. | yatakutaka uandike majibu yako. Kutakuwa na kijisanduku cha kuandika ndani. |
| **5** | If you have a question, or do not understand what to do, let me know. | Kama una swali, au hufahamu cha kufanya, tafadhali niarifu. |
| **6** | Try to answer all test questions. Keep working until you reach the end of the test. Once you finish, you may check your work in this test only. Remember, you can see the directions whenever you need them during the test by clicking the **Question Mark** button in the top right-hand corner of your screen. | Jaribu kujibu maswali yote ya mtihani. Endelea kujibu maswali hadi ufike mwisho wa mtihani. Pindi unapomaliza kujibu maswali, unaweza kukagua kazi yako katika mtihani huu pekee. Kumbuka, unaweza kuona maelekezo wakati wowote mtihani unapoendelea kwa kubofya kitufe cha **Question Mark (Alama ya Kiulizi)** katika kona ya juu kulia ya skrini yako. |
| **7** | When you reach the **Attention** box saying that you have answered all the questions on this test, do not go on, please let me know and I will help you. When you are ready to begin this test, click the **Begin Test Now** button. | Ukifikia kisanduku cha **Attention (Tahadhari)** kinachokuarifu kwamba umejibu maswali yote katika mtihani huu, usiendelee, tafadhali, niarifu nikusaidie. Ukiwa tayari kuanza mtihani huu, bofya kitufe cha **Begin Test Now (Anza Mtihani Sasa)**. |
| **8** | You should now see the **Attention** box that asks you to select the **End Test** button to review your answers. Click **OK** and then the **End Test** button with the red square at the top of your screen. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Attention (Tahadhari)** kinachokuomba uchague kitufe cha **End Test (Tamatisha Mtihani)** ili kuyapitia majibu yako. Bofya kitufe cha **OK** kisha **End Test (Tamatisha Mtihani)** kilicho na mraba mwekundu juu ya skrini yako. |
| **9** | If you are using full screen, select  in the upper-left corner to exit full-screen mode and access the global menu. A message appears, asking for a password. Enter your first name as password and select **OK.** The global menu appears on the top of the screen. | Kama Unatumia skrini nzima, chagua  katika kona ya juu kushoto kuondoka kutoka skrini nzima na kuifikia menyu ya dunia. Ujumbe utakuokuomba nenosiri utajitokeza. Andika jina lako la kwanza kama nenosiri kisha bofya **OK**. Menyu ya dunia itatokea sehemu ya juu ya skrini. |
| **10** | You should now see another **Attention** box saying you have reached the end of the test. Click the **Yes** button. | Unapaswa sasa kuona kisanduku kingine cha **Attention (Tahadhari)** kinachosema umefika mwisho wa mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)**. |
| **11** | If you have marked any items for review, please go back and check these items now. You will not be able to go back to these questions later. | Kama uliweka kando maswali mengine ya kupitia baadaye, tafadhali yapitie sasa. Hutaweza kuyarudia maswali haya wakati mwingine. |
| **12** | If you are sure that you are done with all the questions in this test, please select the **Submit Test** button. | Kama una uhakika kwamba umekamilisha maswali yote katika |

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| | | mtihani huu, tafadhali bofya kitufe cha **Submit Test (Wasilisha Mtihani)**. |
| **13** | You should now see a **Warning** box asking if you are sure you want to submit the test. Click the **Yes** button if you are done. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Warning (Onyo)** kikiuliza kama una uhakika unataka kuwasilisha mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)** ikiwa umemaliza. |
| **14** | You will now see the **Your Results** page. You may click the **Log Out** button now. This screen does not give us any test results. It just confirms that your test was completed and submitted, and is now moving on to be scored. | Sasa utaona ukurasa wa **Your Results (Matokeo Yako)**. Unaweza kubofya kitufe cha **Log Out (Ondoka)** sasa. Skrini hii haitupatii matokeo yoyote ya mtihani. Inathibitisha tu kwamba mtihani wako ulikamilishwa na kutumwa na sasa unaelekezwa hatua ya kutuzwa alama. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21

## SUMMATIVE ASSESSMENT– DIRECTIONS FOR ADMINISTRATION: Speaking

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **1** | This is a Speaking test. It will give you a chance to show how well you can speak in English. You will hear the questions. If you need to hear a question again, click on the **Replay** button. To answer each question, please respond in English to me.<br><br>If you don't understand what to do, please let me know. | Huu ni mtihani wa Kuongea. Utakupa fursa ya kuthibitisha ubora wako wa kuzungumza Kiingereza. Utasikia maswali. Kama unataka kulisikia swali tena, bofya kitufe cha **Replay (Rudia Tena).** Kujibu kila swali, tafadhali nijibu kwa Kiingereza.<br><br>Kama hufahamu cha kufanya, tafadhali niarifu. |
| **2** | Try to answer all test questions. Keep working until you reach the end of the test. Once you finish, you may check your work in this test only. Remember, you can see the directions whenever you need them during the test by clicking the **Question Mark** button in the top right-hand corner of your screen. | Jaribu kujibu maswali yote ya mtihani. Endelea kujibu maswali hadi ufike mwisho wa mtihani. Pindi unapomaliza kujibu maswali, unaweza kukagua kazi yako katika mtihani huu pekee. Kumbuka, unaweza kuona maelekezo unapoyahitaji wakati wa mtihani kwa kubofya kitufe cha **Question Mark (Alama ya Kiulizi)** katika kona ya juu kulia ya skrini yako. |
| **3** | Pause after you answer each question so that I can help you. When you are ready to begin this test, click the **Begin Test Now** button. | Tua baada ya kijibu kila swali ili niweze kukusaidia. Ukiwa tayari kuanza mtihani huu, bofya kitufe cha **Begin Test Now (Anza Mtihani Sasa)**. |
| **4** | You should now see the **Attention** box that asks you to select the **End Test** button to review your answers. Click **OK** and then the **End Test** button with the red square at the top of your screen. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Attention (Tahadhari)** kinachokuomba uchague kitufe cha **End Test (Tamatisha Mtihani)** ili kuyapitia majibu yako. Bofya kitufe cha **OK** kisha **End Test (Tamatisha Mtihani)** kilicho na mraba mwekundu juu ya skrini yako. |
| **5** | If you are using full screen, select  in the upper-left corner to exit full-screen mode and access the global menu. A message appears, asking for a password. Enter your first name as password and select **OK**. The global menu appears on the top of the screen. | Kama Unatumia skrini nzima,  chagua katika kona ya juu kushoto kuondoka kutoka mwonekano wa skrini nzima ili kuifikia menyu ya dunia. Ujumbe utatokea ukikuomba nenosiri{1]. Andika jina lako la kwanza kama nenosiri kisha bofya **OK**. Menyu ya dunia itatokea sehemu ya juu ya skrini. |
| **6** | You should now see another **Attention** box saying you have reached the end of the test. Click the **Yes** button. | Unapaswa sasa kuona kisanduku kingine cha **Attention (Tahadhari)** kinachosema umefika mwisho wa mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)**. |
| **7** | If you have marked any items for review, please go back and check these items now. You will not be able to go back to these questions later. | Kama uliweka kando maswali mengine ya kupitia baadaye, tafadhali yapitie sasa. Hutaweza kuyarudia maswali haya wakati mwingine. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21 

| Track # | English | Swahili |
|---|---|---|
| **8** | If you are sure that you are done with all the questions in this test, please select the **Submit Test** button. | Kama una uhakika kwamba umekamilisha maswali yote katika mtihani huu, tafadhali bofya kitufe cha **Submit Test (Wasilisha Mtihani)**. |
| **9** | You should now see a **Warning** box asking if you are sure you want to submit the test. Click the **Yes** button if you are done. | Sasa unapaswa kuona kisanduku cha **Warning (Onyo)** kikiuliza kama una uhakika unataka kuwasilisha mtihani. Bofya kitufe cha **Yes (Ndio)** ikiwa umemaliza. |
| **10** | You will now see the **Your Results** page. You may click the **Log Out** button now. This screen does not give us any test results. It just confirms that your test was completed and submitted, and is now moving on to be scored. | Sasa utaona ukurasa wa **Your Results (Matokeo Yako)**. Unaweza kubofya kitufe cha **Log Out (Ondoka)** sasa. Skrini hii haitupatii matokeo yoyote ya mtihani. Inathibitisha tu kwamba mtihani wako ulikamilishwa na kutumwa na sasa unaelekezwa hatua ya kutuzwa alama. |

©2022 Regents of the University of California. For permission to use this work, please contact ELPA21